AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Sikukuu katika Australia

## Likizo za shule

Muhula wa shule wa Australia huanza mwishoni mwa mwezi wa Januari/mwanzoni mwa mwezi wa Februari. Kuna muhula nne wa shule, na kila muhula ina muda wa karibu wiki 10. Kila muhula inaishia na mapumziko ya likizo ya shule. Tarehe za kila muhula ni tofauti katika majimbo mbalimbali lakini kwa ujumla kuna mapumziko ya likizo ya wiki mbili karibu Aprili, Julai na Oktoba. Kuna tena mapumziko marefu zaidi ya likizo ya wiki sita mwishoni mwa mwaka wa shule wakati wa majira ya joto (mwishoni mwa mwezi Desemba na Januari).

## Sikukuu za umma

Katika sikukuu za umma, shule na huduma nyingi za serikali zinafungwa. Hata hivyo maduka mengi hukaa wazi. Baadhi za sikukuu za umma ni za kitaifa (katika kote Australia), baadhi ni maalum kwa maeneo mbalimbali katika Australia, na baadhi zake hubadilika tarehe zao kila mwaka.

Hapa ni orodha ya sikukuu za umma kitaifa katika Australia

**Januari 1** – Sikukuu ya Mwaka Mpya (New Years Day). Kuadhimisha mwanzo wa mwaka mpya wa kalenda

**Januari 26** – Siku ya Australia (Australia Day)

**Machi au April** – Good Friday, Sikukuu ya Pasaka (Easter) na Jumatatu ya Pasaka (Easter). Sherehe ya kidini ya wakristo

**April 25** – Siku ya ANZAC. Kuwakumbuka wale ambao walishiriki kwa vita

**June** – Sikukuu ya Kuzaliwa Malkia. Kuadhimisha Malkia wa Uingereza ambaye pia ni Malkia wa Australia

**December 25** – Sikukuu ya Krismasi

**December 26** – Boxing Day. Sherehe ya kijamii kufuata Sikukuu ya Krismasi.









Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM